



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

BARUA ZOTE ZIANDIKWE NA KUTUMWA KWA:

Ofisiya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P. 70, SIKONGE
TABORA

SIMU: 0659 566 703 (Direct line)

Barua Pepe: ded@sikongedc.go.tz

MACHI 23, 2022

TAARIFA KWA UMMA

FURSA ZA UWEKEZAJI WA VIWANDA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

Wilaya ya Sikonge ni moja kati ya Wilaya saba (7) za Mkoa wa Tabora iliyo na eneo la ardhi lenye ukubwa wa kilometa za mraba 27,873, vitongoji 287, vijiji 71, kata 20, tarafa 2.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge inautangazia Umma kuwa kuna fursa za uwekezaji wa Viwanda katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Viwanda (Industrial Parks) kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

Mpaka sasa Wilaya ya Sikonge ina kiwanda kimoja cha kati cha kuchakata na kusindika mazao ya Nyuki katika eneo hilo la viwanda.

SIFA ZA ENEO.

I. UKUBWA

Eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda lina ukubwa wa Hekta 416.66 na lina jumla ya viwanja 103.

ii. BARABARA

Eneo lipo kandokando ya Barabara kuu inayounganisha Mikoa ya Katavi, Mbeya na Tabora mjini yenye kiwango cha lami, Pamoja na usafiri wa treni kwa kuanzia Tabora mjini kuelekea Mikoa mingine.

iii. MAJI NA UMEME

Eneo lina Miundombinu maji ya kutosha na Umeme wa Uhakika kwa matumizi ya viwanda.

iv. UMILIKI.


Eneo la Viwanda limepimwa na linamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.

V. BEI

Viwanja vianauzwa kwa bei ya Tsh.1,700/= kwa Mita moja ya Mraba.

Hivyo basi wananchi wote wenye nia ya kuwekeza katika eneo hilo mnakaribishwa kuwasilisha maombi kwa kujaza fomu za maombi zinazopatikana katika Ofisi ya Mkurugenzi.

Imetolewa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.



.....
YUSUPH HAMZA

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
SIKONGE**

**MKURUGENZI MTENDAJI,
WILAYA - SIKONGE**